

*Shairi lifuatalo limeandikwa na Mshairi Bakari Mwamboga wa Uholanzi, ambaye anazungumzia falsafa ya “Kudra”. Kwa shairi lake anapingana na ile dhana isemayo “Jitihada yashinda Kudra”. Hata hivyo Mheshimiwa Mwamboga, anatumkumbusha kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa yale aliyotujalia, na tuendelee kumuomba, kudra zake kwa yale tunayoyatarajia.*

### **KUJIPA HUWEZI**

- |   |   |
|---|---|
| <p>1. Zingatia waziwazi, usingoje kuambiwa,<br/>Bure ukajipa kazi, na mwisho hutaambuwa,<br/>Apangaye ni mwenyezi, atakalo yeye huwa,<br/>Ambalo hukujaliwa, mja kujipa huwezi</p> <p>2. Sio wako uamuzi, kutaka kitu kikawa,<br/>Wala si wingi wakazi, sababu kufanikiwa,<br/>Ukumbuke kwa mwenyezi, hua ushakubaliwa,<br/>Ambalo hukujaliwa, mja kujipa huwezi</p> <p>3. Tena uwe msikizi, shukuru kifanikiwa,<br/>Sijinaki kwa ufyози, kwamba utakalo huwa,<br/>Wajalia kwa machozi, maisha kuchafukiwa,<br/>Ambalo hukujaliwa, mja kujipa huwezi</p> <p>4. Huna uezо barizi, umshukuru Molewa,<br/>Mola akupa pumzi, na bado hujatambuwa,<br/>Shukurani za mashuzi, wajajuta hili juwa,<br/>Ambalo hukujaliwa, mja kujipa huwezi</p> <p>5. Apangae ni Mwmenyezi, la kuwa na kutokuwa,<br/>Na mwanadamu hawezi, kujipa ila kupewa,<br/>Kupata mja si kazi, kwa Mola wabarikiwa,<br/>Ambalo hukujaliwa, mja kujipa huwezi</p> | <p>6. Unge tamani uzazi, kuzaa ni majaliwa,<br/>Uwe bingwa wa mapenzi, baru baru sawa sawa,<br/>Asipotaka mwenyezi, huzai mwana tambuwa,<br/>Ambalo hukujaliwa, mja kujipa huwezi</p> <p>7. Leo waringia kazi, waringa kuajiriwa,<br/>Wasokazi si wapuzi, nafasi hawaja pewa,<br/>Umepewa na mwenyezi, kushukuru ndio sawa,<br/>Ambalo hukujaliwa, mja kujipa huwezi</p> <p>8. Riziki zake Mwenyezi, kwa viumbe akitowa,<br/>Yeye peke muamuzi, akosae na kupewa,<br/>Mja hili hugeuzi, bure utajisumbuwa,<br/>Ambalo hukujaliwa, mja kujipa huwezi</p> <p>9. Hapa natama utenzi, msojuwa mshajuwa,<br/>Narudi nenda barizi, macho nimewafumbuwa,<br/>Kwa tata siwatatizi, niloyasema ni sawa,<br/>Ambalo hukujaliwa, mja kujipa huwezi</p> |
|---|---|

***B. Mwamboga  
Holland***